Version 3 (05/09/2023)

**Optimizing screening practice for gestational diabetes mellitus in primary healthcare facilities in Tanzania**

**Annex 7: Topic guide – Women interview (IDI) for sub-study 3.**

| **Interview metadata** | |
|---|---|
| Participant ID | |
| Age | |
| Marital status | |
| Education | |
| Employment | |
| Languages spoken | |
| Clinical profile (Gravidity) | |
| Date of the interview | |
| Place of interview | |
| Start time | |
| End time | |

Question guide for IDI

1. How are you today? How is the pregnancy going on?
2. Can you tell me about yourself?
   Prompt – age, gravidity and parity, gestation age (LNMP), marital status, how many children do you have, what do you do (work), education level.
3. Can you please tell me how the day is when you go for your ANC clinic visit?
   Prompt –
   a. time you wake up, time you arrive at the facility, what happens when you arrive at the clinic (registration to consultation to tests)
   b. Health education services provided – who provides it, is enough health education provided, is GDM part of the education topics, do you think more education should be provided on GDM?
   c. Tests conducted – are you aware of what type of tests are done to you and the results when you visit the clinic.
4. Can you please tell me what was different about the last visit for ANC when you came and we met at the clinic?
   Prompt –
   a. The testing process for GDM,
   b. What things you did not like and why?
   c. What things did you like and why?
   d. Is it important to screen for GDM? why?
   e. Was it a good thing that you got tested?
   f. Do you think it should be done to every pregnant woman coming to the clinic?why? if NO why?

5. Can you now please tell me what it was like after being given the results of your GDM
   Prompt –
   a. Changes in diet
   b. Support in medication
   c. Support from spouse and family
   d. The result in reference to the growing baby (positive vs negative)
   e. What challenges did you face after getting the results?
   f. For those who are GDM positive – was it a burden, was it a good information to know it early, was it important to know it early, what was it like to be told having GDM?
6. Concerning screening for GDM at ANC clinic, what things do you think should be improved to make it better?
   Prompt
   a. Education materials and sessions
   b. Type of test
   c. Care after receiving the results
   d. Payments
   e. If it was to be paid for, would you have tested? How much would it be okay for you to test?
7. Do you think all pregnant women should be screened for GDM during ANC visits?why?
8. If you were asked to come in a fasting state (not eating for atleast 8 hours) before visiting the clinic, what will be your reaction
   Prompt
   a. is it possible
   b. what are the challenges in doing that
   c. What can be done to make it more easier
9. Concerning screening for GDM at ANC clinic that you experienced, what good things do you think should be maintained?
10. Before we end our conversation, is there anything else that you would like to share with me concerning what we have been talking about?

**Optimizing screening practice for gestational diabetes mellitus in primary healthcare facilities in Tanzania**

**Annex 7: Muongozo wa mazungumzo – wanawake (IDI) utafiti mdogo namba 3.**

| **Taarifa za mshiriki** | |
|---|---|
| Namba ya mshiriki (ID) | |
| Umri | |
| Hali ya ndoa | |
| Kiwango cha elimu | |
| Hali ya ajira | |
| Lugha unayozungumza | |
| Hali ya ujauzito (Gravidity) | |
| Tarehe ya mahojiano | |
| Sehemu ya mahojiano | |
| Muda wa kuanza mahojiano | |
| Muda wa kumaliza mahojiano | |

Muongozo wa maswali

1. Habari yako leo? Vipi hali ya ujauzito, unaendeleaje?
2. Naomba nielezee kuhusu wewe?
   Maswali ya nyongeza: Umri, hali ya ujauzito, umri wa mimba, hali ya ndoa, una Watoto wangapi, unafanya kazi kazi gani, kiwango chako cha elimu.
3. Nielezee jinsi siku inavyokuwa ukiwa unaenda kliniki ya uja uzito?
   Maswali ya nyongeza:
   a. Muda unao amka, muda unaofika hospitali, nini kinafanyika unapofika hospitali (kuanzia mapokezi vipimo hadi unapo onwa na mtoa huduma na kuondoka)
   b. Elimu ya afya inayotolewa – nani hua anatoa, elimu unayopata inajitosheleza, je sukari ya ujauzito hua inaongelewa, unadhani elimu zaidi kuhusu sukari kwa wajawazito inahitajika kutolewa?
   c. Vipimo gani hua unafanya – unafahamu ni vipimo gani hua unafanya, ni tofauti kati ya kliniki na kliniki, na unaelewa maana ya majibu ya vipimo vyako unavyofanya ukija kliniki? Kitu gani kinaweza kuboreshwa kwenye hili?
4. Naomba nielezee nini kilikua tofauti ile siku tulivyo onana mara ya mwisho ulivyokuja kliniki?
   Maswali ya nyongeza
   a. Vipimo vilivyofanyika na utaratibu wake
   b. Vitu gani hukuvipenda jinsi vilivyofanyika na kwanini?

c. Vitu gani ulivipenda jinsi vilivyofanyika, na kwanini?
d. Kuna umuhimu wowote wa kupima kisukari wakati wa ujauzito, kwanini?
e. Ilikua ni kitu kizuri kupimwa sukari ulivyokuja? Kwanini?
f. Unadhani ni kitu ambacho inabidi kifanyike kwa wajawazito wote wanaokuja kliniki?kwanini? kama Hapana, kwanini?

5. Naomba nielezee ulijisikiaje pindi ulipopata majibu yako ya sukari
   Maswali ya ziada:
   a. Mabadiliko ya "diet"
   b. Dawa
   c. Ushirikiano/mapokeo kwa ndugu na familia baada ya kuwaambia
   d. Majibu na ukuaji wa mtoto (mawazo hasi na chanya kwako yalikua yapi)
   e. Ni changamoto gani ulipata baada ya kupata majibu
   f. Kwa wale ambao majibu yalikua "positive" – ulihisi ni mzigo umeongezewa, ulihisi ni taarifa njema kujua mapema, kulikua na umuhimu wowote kujua hili mapema, ulijisikiaje ulipo ambiwa ni mtu mwenye ugonjwa wa sukari wakati wa ujauzito?
6. Kuhusu huduma ya upimaji wa sukari wakati wa ujauzito, ni vitu gani unadhani vinahitaji maboresho?
   Maswali ya ziada
   a. Vipeperushi vya elimu (viweje)
   b. Utolewaji wa elimu (iwe vipi)
   c. Aina ya vipimo
   d. Huduma baada ya kupima
   e. Malipo
   f. Kama ingalikuwa unatakiwa kulipiwa kipimo cha sukari, ungepima? Ni kiasi gani kingekuwa sawa kwako kulipia kufanya kipimo hiki?
7. Je, unadhani wajawazito wote wanatakiwa kupima sukari wakati wa uja uzito? Kwanini?
8. Kama ungeombwa kuja ukiwa hujala ili ufanye kipimo (kuto kula kwa masaa 8 kabla ya kipimo) ungelichukuliaje hilo swala.
   Maswali ya ziada
   a. Inawezekana
   b. Ni changamoto zipi katika kulifanya hilo
   c. Nini kinaweza kufanyika kulirahisisha hilo
9. Kuhusu huduma ya upimaji wa sukari uliyopata mara ya mwisho ulipokuja kliniki, ni nini kizuri unadhani kinahitaji kuendelezwa ?
10. Kabla ya kumaliza mazungumzo, kuna jambo lolote unataka kuniambia kuhusu mambo yote tuliyokua tunazungumzia hapa?

Version3 (03/08/2023)

**Karatasi ya Taarifa ya Mshiriki wa Utafiti–Wanawake (kwaIDI)**

Unakaribishwa kushiriki katika utafiti wa uchunguzi wa kisukari kwa wajawazito katika vituo vya afya vya msingi nchini Tanzania ambao utafanywa na CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI kwa ushirikiano na Taasisi ya Tropical medicine na Chuo Kikuu cha Antwerp, Ubelgiji.

Hati hii inakupa habari muhimu ambayo ni muhimu ili uweze kuelewa kabla ya kuamua juu ya kushiriki katika utafiti huu. Itakueleza kuhusu haki zako kabla na wakati wa kushiriki katika utafiti huu. Kabla ya kuamua kushiriki au kutoshiriki katika utafiti huu, ni muhimu kuelewa taarifa katika fomu hii, kwa sababu inaelezea haki zako, wajibu wetu kwako, madhumuni, taratibu, faida, hatari na usumbufu unaohusiana na somo hili, na haki ya kukataa au kusitisha ushiriki wako wakati wowote.

Tafadhali, jisikie huru kuuliza maswali yoyote wakati wowote, kwa mfano kuhusu faida inayowezekana na hatari zinazowezekana zinazohusiana na somo hili. Ushiriki wako ni wa hiari. Unaweza kuwasiliana na mtu yeyote unayemwamini juu ya utafiti, na unaweza kuchukua muda wako kufikiria juu ya ushiriki wako. Na pale utakapo amua kushikiriki, weka hizi taarifa na fomu ya idhini katika kipindii chote cha tafiti.

**KUSUDI NA MAELEZO YA TAFITI**

Utafiti huu utatusaidia kujifunza zaidi kuhusu jinsi bora tunavyoweza kuboresha huduma ya uchunguzi wa kisukari wakati wa ujauzito katika hospitali hii. Miongoni mwa huduma ambazo mwanamke mjamzito anastahili kupata wakati anapohudhuria kliniki ni kuchunguzwa kama ana kisukari cha uja uzito, hii ni katika kuhakikisha mama huyu anapata huduma stahiki wakati wa ujauzito.

Kwa tafiti hii, tunalenga kupata kufahamu hali ya ugonjwa wa kisukari miongoni mwa wanawake wajawazito na kupata maoni kutoka kwa watoa huduma ya afya, wasimamizi wa afya na wajawazito jinsi ambavyo uchunguzi bora unaweza kupangiliwa ili kuendana na muktadha wa hospitali hizi.

Tutaweza kupata matokeo kwa kuwapima wanawake wajawazito na kujifunza kutoka kwao na wahudumu wa afya kuhusu uzoefu na mapendekezo yao ili kupata mbinu ya uchunguzi wa utendaji inayopendekezwa. Kufanikisha hili, ni sababu ya kwa nini wewe ni miongoni mwa wanawake 946 ambao wamealikwa kushiriki katika utafiti huu.

Katika utafiti huu, karibu washiriki 960 (wakiwemo watoa huduma za afya na wanawake wajawazito) watashiriki kutoka hospitali mbili tofauti ( Hospitali ya Kisarawe na Hospitali ya Mbagala rangi tatu) nchini Tanzania.

**JINSI UTAFITI UTAKAVYO FANYIKA**

Ukikubali kuwa sehemu ya utafiti huu na kuthibitisha umekidhi masharti ya kushiriki, utaombwa kushiriki katika mahojiano yatakayo chukua kati ya dakika 40 hadi 60. Katika mahojiano hayou totajadili kuhusu hali yako na uzoefu wako tangu mara ya mwisho tulipo onana wiki 4 zilizopita na kupiga sukari. Na nini kinatakiwa kuboreshwa ili huduma ya upimaji wa kisukari wakati wa uja uzito iwe bora zaidi pale hospitali. Tutahakikisha na kukuruhusu pale utakapo hitaji kusimamisha mahojiano kwa ajili ya kuhudumia dharura pale itakapotokea. Na tutahakikisha tunafanya mahojiano yawe mafupi wakati tukihakikisha tunapata taarifa stahiki ili tusichukue muda wako mrefu kutoka kwenye shughuli zako za kila siku.

**HATARI NA USUMBUFU**

Hakuna hatari za moja kwa moja zinazotokana na ushiriki wako katika mahojiano haya. Wakati wa mahojiano, Iwapo utajihisi kutokua tayari kujibu baadhi ya mada/maswali yaliyoulizwa, unaruhusiwa kupuuza na kutojibu swali hilo.

**FAIDA**

Hutapata manufaa yoyote ya moja kwa moja kwa kushiriki katika utafiti huu, hata hivyo maelezo ambayo utashiriki yatachangia mkusanyiko wa maarifa ambayo yatasaidia kuwafahamisha watunga sera kuhusu kuboresha ubora wa hospitali zetu za kliniki ya waja wazito hasa kwa ajili ya uchunguzi wa huduma ya sukari ya wakatii wa uja uzito.

**FIDIA NA BIMA**

Utapokea kiasi kidogo cha Tsh 10,000 kufidia muda wao baada ya kumaliza mahojiano.
Mratibu wa utafiti huu, Taasisi ya Tiba ya Kitropiki, imepata bima ya kufidia madhara au jeraha lolote linaloweza kusababishwa na kushiriki katika utafiti. Iwapo utapata madhara au una maswali kuhusu kuumia kwa matokeo ya kuwa katika utafiti, tafadhali wasiliana naDrAmaniKikula0714753852

**ULINZI WA FARAGHA**

Tutafanya kila jambo linalowezekana kulinda usiri wa taarifa zako. Taarifa zinazokuhusu zitatunzwa kwa usiri kabisa; Tutahifadhi taarifa za kielektroniki kwenye kanzi data ambayo itakutambua kwa kutumia msimbo na sio jina lako. Nyaraka ambazo jina lako limetajwa hazitashirikishwa na mtu yeyote, isipokuwa watafiti wa utafiti, na watu wengine wachache ambao wanapaswa kuitunza kwa siri, na uwakilishi wa chuo kikuu Antwerp na ITM. Kwa kutia saini fomu hii ya kibali uliyopewa unakubaliana na taarifa hii ya utunzwaji wa rekodi zako.
Taarufa zote zitahifadhiwa kwa kipindi cha miaka 5 baada ya kuchapishwa. Matokeo ya utafiti yatachapishwa katika majarida (ya kitabibu). Taarifa yako inaweza kushirikishwa na watafiti wengine kwa ajili ya utafiti wa siku za usoni, baada ya kuondoa utambulisho (kumaanisha kuwa hawawezi kuunganisha tena na jina lako: hakuna mtu atakayejua zaidi kwamba taarifa hizi ni za kwako.
Jina lako halitaonekana katika hifadhi data yoyote, ripoti au uchapishaji unaotokana na utafiti huu.
Kwa mujibu wa Kanuni ya Ulinzi wa Data ya Ulaya (GDPR), unaweza kuomba kurejea na kusahihisha taarifa yako ya kibinafsi ikiwa inahitajika.

**KUSHIRIKI KWA HIARI**

Kushiriki kwako katika utafiti huu ni kwa hiari kabisa. Ni chaguo lako kama ungependa kushiriki katika tafiti hii. Kama umechagua kushiriki au kutoshiriki, huduma zote unazopata kwenye kliniki hii zitabaki vile vile. Pia una haki ya kusitisha ushiriki wako katika utafiti wakati wowote, hata baada ya kuwa umetia saini kwenye Fomu ya Ridhaa Iliyoarifiwa. Huna sababu ya kutoa sababu ya kusitisha ushiriki wako.
Pia mtafiti anaweza kuamua kusitisha ushiriki wako katika utafiti huu wakati wowote vilevile, bila kukuuliza kibali chako, iwapo ataona ni heri zaidi kwako. Hili likitokea, mtafiti atakueleza hili, na kujadili kitakachotokea baadaye.

MTU WA KUWASILIANA NAE KWA MASWALI

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu ushiriki wako katika utafiti huu, haki zako au ikiwa unafikiri umedhuriwa kutokana na utafiti, unaweza kuwasiliana, sasa, wakati, au baada ya utafiti:
Dr Amani I. Kikula 0714753852 AU
Dr Nahya Salim
+255713250074
AU
Mwenyekiti, kamati ya maadili ya tafiti katika taasisi ya NIMR, P. O. Box 9653 Dar es Salaam, Tanzania; Telephone & Fax: Tel: +255 22 2121400, Fax: 255 22 2121360 E- Mail: ethics@nimr.or.tz
Utapata nakala ya fomu hii

Version3 (03/08/2023)

**Hati za idhini–Wanawake IDI**

Nimepokea nakala ya karatasi ya taarifa na ninaelewa kikamilifu mada ya utafiti huu, upeo wa mchango wangu, na haki yangu ya kukataa kushiriki au kujiondoa kwenye utafiti wakati wowote. Ninakubali kwa uhuru kushiriki katika utafiti huu na kushirikiana katika mahojiano/shughuli za utafiti. Nakubali timu ya utafiti kutumia maelezo yangu ya kimatibabu kutoka kwa rekodi za utunzaji katika ujauzito. Faida na hatari zinazowezekana za kushiriki katika utafiti huu zimeelezwa na nimeridhika. Ushiriki wangu katika tafiti hii ni wa hiari na kwamba niko huru kutoka kutoka kwenye kipindi chochote na wakati wowote. Ninakubali kutoa mawasiliano kwa ajili ya kukumbushwa tarehe ya mahojiano. Naelewa hilo jina langu,nambari ya simu na anwani itatenganishwa na taarifa ambazo zitolewa kwa watu wengine katika utafiti.
Nathibitisha kupokea 10,000 Tsh kutoka kwa mtafiti.

| | |
|---|---|
| **Tarehe** | _____/_____/__________ |
| **Herufi za majina (initials)** | ______________________________ |
| **Sahihi( au alama ya dole gumba)la mshiriki** | ______________________________ |

**Kukamilishwa na watafiti watakao chukua taarifa za kibali**

Mimi ninatia saini, ………………………………………………………………………… nathibitisha kuwa nimemfahamisha mshiriki (na/au mzazi/mlezi wa kisheria) kuhusu vipengele vyote muhimu vya utafiti huu. Ninathibitisha kwamba amekubali kwa hiari yake kushiriki katika utafiti.

| | |
|---|---|
| **Tarehe** | _____/_____/__________ |
| **Sahihi ya mtafiti** | ______________________________ |
| **Jina la mtafiti** | |